**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA STASHAHADA YA UALIMU WA SEKONDARI (DSEE) 2018

# 721 LUGHA YA KISWAHILI

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA STASHAHADA YA UALIMU WA SEKONDARI (DSEE) 2018

# 721 LUGHA YA KISWAHILI

*Kimechapishwa na;*

Baraza la Mitihani la Tanzania,

S.L.P 2624, Dar es Salaam,

Tanzania.

**©Baraza la Mitihani la Tanzania, 2018**

**Haki zote zimehifadhiwa**

## YALIYOMO

DIBAJI ..... iv
1.0 UTANGULIZI ..... 1
2.0 TATHMINI YA KILA SWALI ..... 2
2.1 SEHEMU A: TAALUMA NA UTAALAMU ..... 2
2.1.1 Swali la 1: Uhakiki wa Fasihi Andishi ..... 2
2.1.2 Swali la 2: Zana za Kufundishia na Kujifunzia ..... 5
2.1.3 Swali la 3: Utumizi wa msamiati na miundo ya Kiswahili ..... 7
2.1.4 Swali la 4: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia ..... 9
2.1.5 Swali la 5: Ufahamu ..... 12
2.1.6 Swali la 6: Vifaa vya Mtalaa wa Somo la Kiswahili ..... 14
2.1.7 Swali la 7: Matamshi na Lafudhi ya Kiswahili ..... 17
2.1.8 Swali la 8: Maendeleo ya Kiswahili ..... 20
2.1.9 Swali la 9: Upimaji ..... 23
2.1.10 Swali la 10: Upimaji ..... 26
2.2 SEHEMU B: TAALUMA ..... 30
2.2.1 Swali la 11: Fasihi ..... 30
2.2.2 Swali la 12: Uhakiki wa Kazi za Fasihi ..... 35
2.2.3 Swali la 13: Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili ..... 41
2.3 SEHEMU C: UTAALAMU ..... 45
2.3.1 Swali la 14: Zana za Kujifunzia na Kufundishia Somo la Kiswahili ..... 45
2.3.2 Swali la 15: Mbinu za Kujifunzia na Kujifunzia Somo la Kiswahili ..... 50
2.3.3 Swali la 16: Ufundishaji wa Mada Teule za Somo la Kiswahili ..... 57
3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU CHA WATAHINIWA KWA MADA ..... 62
4.0 HITIMISHO ..... 64
5.0 MAPENDEKEZO ..... 65
KIAMBATISHO A ..... 66
KIAMBATISHO B ..... 67

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania lina furaha kuupatia umma kitabu hiki kama taarifa ya mrejesho juu ya kufaulu kwa walimu tarajali, wakufunzi, wazazi, waandaaji wa sera na wadau wote wa elimu kwa ujumla katika kutekeleza malengo ya elimu nchini Tanzania.

Kitabu hiki ni tathmini ya mwisho inayoonesha mafanikio ya mfumo wa elimu kwa ujumla hasa katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Kimsingi, uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani huu unaonesha dhahiri namna mfumo wa elimu ulivyofaulu au kushindwa kuwapa watahiniwa maarifa walipokuwa katika mafunzo ya Stashahada ya Ualimu wa Sekondari.

Taarifa hii inaweka bayana sababu za watahiniwa kupata alama za juu, alama za wastani au alama hafifu katika mtihani huu. Vilevile, taarifa hii inaonesha baadhi ya sababu zilizowafanya watahiniwa wengi kufanya vizuri. Aidha, sababu za baadhi ya watahiniwa kupata alama hafifu katika majibu yao zimefafanuliwa. Miongoni mwa sababu hizo ni kushindwa kuelewa matakwa ya swali, uwezo mdogo wa watahiniwa katika kuelewa mada iliyotahiniwa na uwezo mdogo wa watahiniwa kujieleza kwa ufasaha.

Kwa mantiki hiyo, Baraza la Mitihani la Tanzania linatarajia kuwa taarifa hii itakuwa nyenzo muhimu kwa viongozi wa elimu, viongozi wa shule, wakufunzi na walimu tarajali katika kupata mbinu sahihi za kuboresha viwango vya kufaulu vya watahiniwa katika mitihani ijayo inayoendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa wakufunzi, walimu tarajali na umma kwa ujumla, ambayo yatatumika katika kuboresha taarifa za watahiniwa zitakazofuata.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kuwashukuru Maafisa Mitihani, wakufunzi wa somo na wengine wote waliohusika kutayarisha taarifa hii. Aidha, Baraza linapenda kutoa shukurani zake za pekee kwa wafanyakazi wa Idara ya Utafiti na Tathmini pamoja na Idara ya Huduma za Kompyuta kwa kushiriki katika uchakataji wa data zilizotumika katika taarifa hii.



Dkt. Charles Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua kufaulu kwa watahiniwa kwa kila swali katika mtihani wa Stashahada ya Ualimu wa Sekondari kwa somo la Kiswahili uliofanyika Mei, 2018. Mtihani huu ulikuwa na jumla ya maswali kumi na sita (16) yaliyogawanyika katika sehemu A, B na C kwa kuzingatia mada za *Taaluma* na *Utaalamu*.

Sehemu A ilikuwa na maswali kumi (10) ya majibu mafupi. Maswali hayo yalitolewa katika mada za muhtasari wa Taaluma na Utaalamu. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Kila swali lilikuwa na alama nne (4), hivyo kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama arobaini (40).

Sehemu B ilikuwa na jumla ya maswali matatu (3) ya insha. Maswali haya yalihusu mada za Kitaaluma. Kila swali lilikuwa na alama kumi na tano (15) na mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili (2) tu. Kwa hiyo, sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama thelathini (30).

Aidha, sehemu C ilikuwa na jumla ya maswali matatu (3) ya insha. Maswali hayo yalihusu mada za Utaalamu tu. Kila swali lilikuwa na alama (15) na mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili (2) tu. Hivyo, sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama thelathini (30).

Hali kadhalika, mtihani huu ulikuwa na viwango vitatu vya kufaulu ambavyo ni kiwango kizuri kilichoanzia alama 70 hadi 100, kiwango cha wastani kilichoanzia alama 40 hadi 69 na kiwango hafifu ambacho kilianzia alama 0 hadi 39.

Jumla ya watahiniwa waliosajiliwa kufanya mtihani wa 721 Kiswahili kwa mwaka 2018 walikuwa 320. Kati yao, watahiniwa 319 ndio waliofanya mtihani. Kiwango cha kufaulu cha watahiniwa kwa somo hili kilikuwa kizuri, kwani asilimia 100 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walifaulu kwa daraja A hadi D. Aidha, hapakuwa na watahiniwa walioshindwa kufikia daraja D. Sehemu inayofuata ni tathmini ya kila swali ambapo viwango vya watahiniwa vinaonekana bayana.


## TATHMINI YA KILA SWALI

## 1.1 SEHEMU A: TAALUMA NA UTAALAMU

### 1.1.1 Swali la 1: Uhakiki wa Fasihi Andishi

Swali lilitoka katika mada za Kitaaluma hususan mada kuu ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi*. Swali lililenga kupima ufahamu wa mtahiniwa juu ya sifa za mwandishi wa fasihi ya Kiswahili. Mtahiniwa alitakiwa kueleza kwa kifupi sifa nne za mwandishi wa fasihi ya Kiswahili. Swali lilikuwa na jumla ya alama 4.

Swali lilijibiwa na asilimia 100 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa kiwango cha wastani, kwani asilimia 53.7 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani na zaidi. Chati namba 1 inafafanua viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.





**Chati Namba 1**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 46.4 walipata alama hafifu ambazo ni kuanzia 0 hadi 1.5. Baadhi yao walishindwa kuelewa matakwa ya swali na wengine hawakumudu vizuri mada iliyotahiniwa katika swali hili. Mathalani, baadhi yao walieleza sifa ambazo ni za mwandishi wa fasihi yoyote ile badala ya kueleza kwa kifupi sifa za mwandishi bora wa fasihi ya Kiswahili. Watahiniwa wengine

walieleza hoja moja kwa kurudiarudia. Kielelezo 1.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyekuwa na uelewa mdogo juu ya mada iliyotahiniwa na kuandika sifa moja ya mwandishi wa fasihi ya Kiswahili kisha akairudiarudia na kupata alama 1.

**Kielelezo 1.1**


1. Mwandishi wa fasihi ya Kiswahili anataki
wa awe mahiri wa lugha ya Kiswahili, Awe
ajue Kiswahili fasaha.
Mwandishi wa fasihi ya Kiswahili anatak-
iwa awe na taaluma ya lugha ya
Kiswahili; kwani hii husaidia kuteua
maneno ya Kiswahili kwa ufasaha Amerudia
Mwandishi wa lugha ya Kiswahili
anatakiwa awe mahiri wa lugha ya
Kiswahili.
Anatakiwa awe na ujuzi wa
lugha ya Kiswahili. Mwandishi wa kazi
ya fasihi ya Kiswahili anatakiwa awe na ujuzi;

**Kielelezo 1.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu kwa kurudiarudia jibu sahihi moja badala ya kuelezea sifa nne za mwandishi wa fasihi ya Kiswahili.

Vilevile, asilimia 38.9 walipata alama za wastani ambazo ni kuanzia 2 hadi 2.5. Hawa ni wale walioweza kueleza kwa ufasaha sifa mbili za mwandishi wa kazi za fasihi ya Kiswahili.

Asilimia 14.7 ya watahiniwa waliojibu swali hili walijibu vizuri na walipata alama za juu kuanzia 3 hadi 4. Baadhi yao waliweza kueleza kwa ufasaha sifa nne za mwandishi wa fasihi ya Kiswahili ambazo ni *ajue vizuri hadhira yake, awe na uwezo wa kutumia lugha, awe mbunifu na awe na mpangilio mzuri wa matukio*. Uwezo huo ulitokana na kuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi* na kuelewa matakwa ya swali. Kielelezo 1.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri na kupata alama 4.

**Kielelezo 1.2**

6\. i/ Awe vizuri hadhira yake, Mwandishi wa kazi ya fasihi anatakiwa awe ni mtu anayeijua hadhira yake vizuri kama ni watoto, vijana wazee na aandike kulingana na hadhira yake ilivyo kwa kuangalia uchumi wao, utamaduni wao na utamaduni wao.

ii/ Awe mahiri katika kutumia lugha, mwandishi wa fasihi simulizi awe na uwezo wa kutumia lugha vizuri kwa kufuata kanuni zote za lugha kiswahili.

iii/ Mwandishi anatakiwa awe mubunifu, katika hili mwandishi anatakiwa abuni visa ambavyo vinavuta hisia za wasomaji na kumfanya msomaji kuendelea kusoma fasihi hiyo. ~~hiyo~~


iv/ Awe na mpangilio mzuri wa kazi yake, mwandishi mzuri lazima apange kazi yake katika mtiririko na mpangilio mzuri ambao unamvutia msomaji.

**Kielelezo 1.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali kwa kueleza kwa kifupi sifa nne za mwandishi wa fasihi ya Kiswahili.

### 1.1.2 Swali la 2: Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Swali hili lilitoka katika mada za Kitaalamu hususan mada ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili*. Swali lilimtaka mtahiniwa aeleze kwa kifupi sifa kuu nne za zana bora za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 4.

Asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili na ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Asilimia 93.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani na zaidi. Chati namba 2 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kiasilimia.




**Chati Namba 2:** Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 71.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walijibu vizuri. Wengi wao walipata alama zote 4 kwa kuwa waliweza kuelezea vizuri sifa nne za zana bora za kujifunzia na kufundishia somo la Kiswahili ambazo ni *lazima iwe nadhifu, iendane na mada husika, iwe kubwa kulingana na idadi ya wanafunzi na yenye kujenga kumbukumbu*. Hii inadhihirisha kwamba watahiniwa hao waliimudu vizuri mada ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili*. Kielelezo 2.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama 4.

**Kielelezo 2.1**


2. kueleza kwa kifupi sifa kuu nne za zana bora za kufundishia na kujifunzia,
i/ Lazima iwe nadhifu na yenye kuwavutia wanafunzi wote darasani',
ii/ Lazima iendane na mada au mada ndogo inayotarajiwa kuwasilishwa darasani,
iii/ Kama ni ya maono, hivyo iwe kubwa kiasi' ili kila Mwanafunzi aweze kuiona Vizuri',
iv/ Pia zana bora ni ile yenye kujenga kumbukumbu za kuduma kwa Mwanafunzi kutokana na kile alichojifunza.

**Kielelezo 2.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza vizuri sifa nne za zana bora za kujifunzia na kufundishia somo la Kiswahili.

Vilevile, asilimia 22.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5. Hawa waliweza kueleza sifa mbili za zana bora za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili wakati matakwa ya swali yalikuwa ni sifa nne. Wengine walitaja tu sifa hizo bila kuzitolea maelezo mafupi kama swali lilivyotaka.

Kwa upande mwingine, asilimia 6.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5. Hawa walishindwa kueleza sifa za zana bora za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili kutokana na kushindwa kuelewa vizuri matakwa ya swali. Kwa mfano, baadhi yao walieleza umuhimu wa zana bora badala ya sifa za zana bora za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili. Vilevile wengine walitaja mambo ya kuzingatia wakati wa uandaaji wa zana bora. Umuhimu wa zana bora ulioelezewa ni *hufanya mwalimu apendwe, hukuza uelewa wa wanafunzi, ni rahisi kuibeba na iwe ya kuvutia ujifunzaji* badala ya sifa za zana bora za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili ambazo ni *lazima iwe nadhifu, iendane na mada husika, iwe kubwa kulingana na idadi ya wanafunzi na yenye kujenga kumbukumbu*. Kielelezo 2.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetaja umuhimu wa zana bora za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili badala ya kueleza sifa zake na kupata alama 0.

**Kielelezo 2.2**


2. (i) Hufanya mwalimu apendwe.
(ii) Hukuza uelewa wa wanafunzi.
(iii) Ni rahisi kuibeba.
(iv) Iwe ya kuvutia ujifunzaji.


**Kielelezo 2.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetaja umuhimu wa zana za kufundishia na kujifunzia badala ya sifa za zana bora za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili.

### 1.1.3 Swali la 3: Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili

Swali hili lilitoka katika mada za Kitaaluma na lilihusu mada ya *Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili,* hususan mada ndogo ya *Uambishaji*. Swali lilikuwa na vipengele vinne; (a), (b), (c) na (d) ambapo katika kila kipengele mtahiniwa alitakiwa kueleza kazi moja ya kiambishi kilichopigiwa mstari.

Katika kipengele (a) mtahiniwa alitakiwa kueleza kazi ya kiambishi *–me-* katika tungo "Amejikata kidoleni." Kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa aeleze kazi ya kiambishi *–ya-* katika tungo "Maswali aliyoyajibu." Kipengele (c) kilimtaka mtahiniwa aeleze kazi ya kiambishi *–ki-* katika tungo "Alikiona asubuhi." Kipengele (d) kilimtaka mtahiniwa aeleze kazi ya kiambishi *a-* kama kilivyotumika katika tungo "Anaimba vizuri".


Swali lilijibiwa na asilimia 100 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani na lilikuwa miongoni mwa maswali ambayo yalijibiwa kwa kiwango cha wastani. Asilimia 57.3 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani na zaidi. Chati namba 3 inaonesha viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Namba 3:** Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 42.7 ya watahiniwa walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5. Baadhi yao walishindwa kuelewa matakwa ya swali kwa sababu walieleza kazi za jumla za viambishi vilivyopigiwa mstari badala ya kueleza kazi mahususi ya kila kiambishi kilichopigiwa mstari. Kwa mfano, kuna waliojibu kuwa kazi ya kiambishi "a-" katika kipengele (d) ni kuonesha nafsi badala ya kubainisha kuwa ni nafsi ya tatu umoja. Kielelezo 3.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kulingana na matakwa ya swali na kupata alama hafifu.

**Kielelezo 3.1**





**Kielelezo 3.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu kwa kuwa alitaja kazi za jumla badala ya kueleza kazi mahususi kwa kila kiambishi.

Vilevile asilimia 32 ya watahiniwa waliojibu swali hili, waliopata alama za wastani. Hawa walimudu kujibu vipengele viwili kati ya vinne vilivyohitajika. Aidha, wengine walitoa maelezo ambayo si kamilifu na kupata nusu ya alama kwa kila kipengele.

Aidha, asilimia 25.3 ya watahiniwa walijibu swali hili vizuri kwa sababu waliweza kueleza vizuri kazi mahsusi za viambishi walivyoulizwa katika vipengele vyote vinne. Hii inadhihirisha kwamba watahiniwa wa kundi hili walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili*. Kielelezo 3.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri na kupata alama 3.5.

**Kielelezo 3.2**



3. a) Amejikata kidole
me- kumaana ya kuonesha wa-
kati au cheo.
b) Maswali aliyoyajibu
ya- kuonesha idadi
c) Alikiona asubuhi
-ki- kumaanisha/kuonesha we-
jeshi
d) Anaimba vizuri
A- kiambishi awali nafsi ya
tatu umoja.

**Kielelezo 3.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kueleza kazi za viambishi vilivyopigiwa mstari katika sentensi.

### 1.1.4 Swali la 4: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia

Swali hili lilitoka katika mada za Kitaalamu hususan mada kuu ya *Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili*. Swali lilihitaji mtahiniwa abainishe mada nne za somo la Kiswahili katika shule za sekondari zinazoweza kufundishwa kwa mbinu ya ziara. Swali lilikuwa na jumla ya alama 4.


Asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili na ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Miongoni mwao, asilimia 85.5 walipata alama za wastani na zaidi. Chati namba 4 inafafanua viwango vya kufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Namba 4**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 46.5 ya watahiniwa waliojibu swali hili, walijibu vizuri. Kati yao, kuna waliopata alama zote 4 kwa sababu waliweza kubainisha mada nne za somo la Kiswahili zinazoweza kufundishwa kwa mbinu ya ziara kwa usahihi. Mbinu walizobainisha ni pamoja na *kukua na kuenea kwa Lugha ya Kiswahili, chimbuko la asili ya Lugha ya Kiswahili, matumizi ya Lugha katika miktadha mbalimbali na mawasiliano katika Lugha mazungumzo na Lugha ya maandishi*. Hii inaonesha kuwa wana uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili.* Kielelezo 4.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama 4.

**Kielelezo 4.1**


4 1. KUKUA NA KUENEA KWA LUGHA YA KISWAHILI.
Kufanya ziara katika baadhi ya sehemu zilizojengwa na wamisionari na madrasa zilizojengwa na waarabu. Kwa mfano, Pugu, Tabora boys, Peramiho.

2. CHIMBUKO NA ASILI YA LUGHA YA KISWAHILI.
Kwa mfano kufanya ziara kwenye miji wa Kilwa na kupata maelezo mbalimbali ya watu wanaopatikana hapo ambao wanajua vizuri historia ya mji huo. Pia kufanya ziara katika maktaba mbalimbali kupata nyaraka na vitabu mbalimbali kama vile Utenzi wa mwana-kupona na Safari ya Marco polo.

3. MATUMIZI YA LUGHA KATIKA MIKTADHA MBALIMBALI.
Kwa mfano katika mada ndogo kama vile ishara unaweza kufanya ziara ya kanisani au mahakamani ili kubaini ishara kwa vitendo na sio maneno.

4. MAWASILIANO KATIKA LUGHA YA MAZUNGUMZO NA LUGHA YA MAANDISHI.
Mfano kutokana na mada ndogo ya matumizi ya lafudhi unaweza kufanya ziara katika mikoa mingi ili upate kubaini lafudhi zinazotumika na ufasaha wake.


**Kielelezo 4.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kubainisha mada nne za somo la Kiswahili zinazoweza kufundishwa kwa mbinu ya ziara.

Watahiniwa wengine ambao ni asilimia 39 waliweza kubainisha vizuri mada mbili za somo la Kiswahili ambazo zinaweza kufundishwa kwa kutumia mbinu ya ziara. Aidha, wengine hawakutoa maelezo yanayobainisha vizuri mada za somo la Kiswahili zinazoweza kufundishwa kwa mbinu ya ziara. Hivyo, walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5.

Aidha, asilimia 14.5 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5 kwa kuwa walishindwa kubainisha mada za somo la Kiswahili zinazoweza kufundishwa kwa mbinu ya ziara kwa sababu

walikosa uelewa juu ya mada ya *Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili*. Mathalani, baadhi ya watahiniwa walibainisha mada za masomo mengine kwa mfano, *vyanzo vya nishati, umeme, utalii na vyanzo vya kihistoria* badala ya mada za somo la Kiswahili ambazo ni *kukua na kuenea kwa Lugha ya Kiswahili, chimbuko la asili ya Lugha ya Kiswahili, matumizi ya Lugha katika miktadha mbalimbali na mawasiliano katika Lugha mazungumzo na Lugha ya maandishi* . Kielelezo 4.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kubainisha mada za somo la Kiswahili zinazoweza kufundishwa kwa kutumia mbinu ya ziara.

**Kielelezo 4.2**




**Kielelezo 4.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyebainisha mada za masomo mengine badala ya mada za somo la Kiswahili zinazoweza kufundishwa kwa mbinu ya ziara.

### 1.1.5 Swali la 5: Ufahamu

Swali hili lilitoka katika mada za Kitaaluma hususan mada kuu ya *Ufahamu*. Mtahiniwa alitakiwa kuorodhesha kanuni nne za kuzingatia wakati wa kusoma kwa sauti. Swali lilikuwa na jumla ya alama 4.


Asilimia 100 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walijibu swali hili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri, kwani asilimia 71.1 ya watahiniwa walipata alama za wastani na zaidi. Chati namba 5 inafafanua viwango vya kufaulu kwa asilimia.




**Chati Namba 5:** Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 41.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walijibu vizuri kwa sababu waliweza kuorodhesha kanuni nne za kuzingatia wakati wa kusoma kwa sauti kama vile *sauti inayosikika vizuri, matamshi sahihi, alama za uandishi na kusoma kwa umakini*. Uwezo huo unadhihirisha kwamba watahiniwa wa kundi hili walielewa matakwa ya swali ipasavyo na kuyazingatia. Kielelezo 5.1 ni majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri kulingana na matakwa ya swali.

**Kielelezo 5.1**



5. i) Alama za uandishi
ii) Matamshi
iii) Sauti
iv) Kusoma kwa makini


**Kielelezo 5.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuorodhesha kanuni nne za kuzingatia wakati wa kusoma kwa sauti.

Watahiniwa wengine walishindwa kuorodhesha kikamilifu kanuni nne za kuzingatia wakati wa kusoma kwa sauti. Hawa ni asilimia 29.5 ya

watahiniwa wote waliofanya swali hili na walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5.

Aidha, asilimia 28.9 ya watahiniwa walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5 kwa sababu hawakuelewa matakwa ya swali. Baadhi yao walishindwa kuorodhesha kanuni nne za kuzingatia wakati wa kusoma kwa sauti badala yake waliorodhesha kanuni za jumla za kuzingatia katika ufundishaji na ujifunzaji darasani. Kanuni za jumla za kuzingatia katika ufundishaji na ujifunzaji darasani zilizotajwa ni pamoja na *kuangalia ukubwa wa darasa, uelewa wa wanafunzi, umri wa wananfunzi na hali ya wanafunzi* badala ya kanuni nne za kuzingatia wakati wa kusoma kwa sauti ambazo ni sauti *inayosikika vizuri, matamshi sahihi, alama za uandishi na kusoma kwa umakini*. Aidha, wengine walikwenda kinyume cha matakwa ya swali kutokana na uelewa mdogo juu ya mada ya *Ufahamu.* Kielelezo 5.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi na kupata alama 0.

**Kielelezo 5.2**



5 i/ Kuangalia ukubwa wa darasa
ii/ Uelewa wa wanafunzi
iii/ Umri wa wanafunzi
iv/ Hali ya wanafunzi

**Kielelezo 5.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza kanuni za jumla za kuzingatia katika ufundishaji na ujifunzaji darasani badala ya kanuni nne za kuzingatia wakati wa kusoma kwa sauti.

### 1.1.6 Swali la 6: Vifaa vya Mtalaa wa Somo la Kiswahili

Swali hili lilihusu mada za Kitaalamu hususan, katika mada kuu ya *Vifaa vya Mtalaa wa Somo la Kiswahili*. Swali lilihitaji mtahiniwa aoneshe sifa nne za kiongozi cha mwalimu. Swali lilikuwa na jumla ya alama 4.


Asilimia 100 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walijibu swali hili na ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Asilimia 92.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani na zaidi. Chati namba 6 inaonesha viwango vya kufaulu kwa asilimia.




**Chati Namba 6:** Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 67.7 ya watahiniwa walijibu vizuri swali hili kwa sababu walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili.* Aidha, watahiniwa hawa walielewa vizuri matakwa ya swali. Walifanikiwa kuonesha vizuri sifa nne za kiongozi cha mwalimu ambazo ni *kiwe na majibu ya maswali ya mazoezi yaliyopo, kionyeshe mbinu bora za kufundishia, kionyeshe zana bora za kufundishia na kionyeshe mpangilio maalum wa mada.* Kielelezo 6.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali na kupata alama 4.

**Kielelezo 6.1**



6. i) Kiwe na majibu ya maswali na mazoezi yaliyomo katika kitabu cha mwanafunzi (kitabu cha kiada)

ii) Kionyeshe mbinu bora za kufundishia mada husika katika somo

iii) Kionyeshe zana bora zinazofaa kutumika katika kufundishia mada husika


iv) Kionyeshe mpangilio maalumu wa mada za kufundisha somo husika.

**Kielelezo 6.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuonesha sifa nne za kiongozi cha mwalimu.

Vilevile, asilimia 24.5 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu waliweza kupata alama za wastani ambazo ni kuanzia 2 hadi 2.5 kwa kuwa hawakutoa majibu toshelevu. Mathalani, kuna baadhi ya watahiniwa waliweza kuonesha sifa mbili za kiongozi cha mwalimu na wengine walichanganya sifa za kiongozi cha mwalimu na umuhimu wa kiongozi cha mwalimu.

Aidha, asilimia 7.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu ambazo ni kuanzia 0 hadi 1.5. Baadhi yao hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Vifaa vya Mtalaa wa Somo la Kiswahili*. Wengine walichanganya sifa za kiongozi cha mwalimu na zile za kitabu chochote kwa kuwa hawakuelewa matakwa ya swali. Sifa za kitabu chochote zilizooneshwa na watahiniwa wa kundi hili ni pamoja na *kiwe kimesanifishwa na kuteuliwa na taasisi ya elimu, kijitosheleze kimsamiati, kiwe na jalada linaloonesha mtunzi na kisiwe na karatasi ngumu* badala ya sifa za kiongozi cha mwalimu ambazo ni *kiwe na majibu ya maswali ya mazoezi yaliyopo, kionyeshe mbinu bora za kufundishia, kionyeshe zana bora za kufundishia na kionyeshe mpangilio maalum wa mada*. Kielelezo 6.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa kuonesha sifa nne za kitabu chochote badala ya kiongozi cha mwalimu.

**Kielelezo 6.2**


6(i) lazima kiwe kimesanifishwa na kuteuliwa na taasisi ya Elimu

(ii) Lazima kiwe kimejitosheleza kimsamiati, Maswali na Majibu,

(iii) Lazima kiwe na jarada linaloonyesha utunzi na Mambo yaliyomo

(iv) Ni lazima au kisiwe na karatasi ngumu


**Kielelezo 6.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuonesha sifa nne za kiongozi cha mwalimu badala yake amechanganya na sifa za kitabu chochote.

### 1.1.7 Swali la 7: Matamshi na Lafudhi ya Kiswahili

Swali hili lilitoka katika mada za Kitaalamu hususan mada kuu ya *Matamshi na Lafudhi ya Kiswahili*. Swali lilikuwa na vipengele vinne; (a), (b), (c) na (d) ambapo katika kila kipengele mtahiniwa alitakiwa kutoa maana ya dhana za kifonolojia alizopewa kwa kutumia mifano.

Katika kipengele (a) mtahiniwa alitakiwa kutumia mifano kutoa maana ya dhana ya "vipasuo." Katika kipengele (b) mtahiniwa alitakiwa kutumia mifano katika kutoa maana ya dhana ya "vikwamizi." Vilevile, kipengele (c) kilimtaka mtahiniwa atumie mifano katika kutoa maana ya dhana ya "nazali." Hali kadhalika, kipengele (d) kilimtaka mtahiniwa kutumia mifano katika kutoa maana ya dhana ya "viyeyusho."


Swali hili lilijibiwa na asilimia 85.6 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vibaya kwani asilimia 5.5 pekee ya watahiniwa waliojibu swali hili, ndio walipata alama za wastani na zaidi. Chati namba 7 inafafanua viwango vya kufaulu kwa asilimia.




**Chati Namba 7:** Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 94.5 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu ambazo ni kuanzia 0 hadi 1.5. Watahiniwa hawa walikosa uelewa juu ya mada ya *Matamshi na Lafudhi ya Kiswahili* kwa sababu hata waliojaribu kujibu swali hili walijikuta wakieleza maana ya dhana hizo bila kuzihusisha na dhana ya fonolojia. Wengine walishindwa kutimiza matakwa ya swali kwa kutokuweka mfano katika maelezo ya kila dhana na wengine waliandika mambo yasiyohusiana kabisa na fonolojia, kwa mfano kuna mtahiniwa mmoja alitoa maana ya vipasuo kuwa *ni mofimu zinazoweza kukamilisha maana ya neno katika lugha, yaani huweza kuwekwa mwanzo au mwisho wa mzizi wa neno* badala ya *vipasuo ni sauti za Lugha ambazo hutolewa na binadamu ambapo ala za sauti huwa zimefunga mkondo wa hewa na kuachia kwa ghafla, kwa mfano sauti/p/, /b/ na /d/. Kielelezo* 7.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kueleza maana ya dhana katika kipengele (a) hadi (d) kutokana na kukosa maarifa ya kutosha juu ya mada ya *Matamshi na Lafudhi ya Kiswahili* na kupata alama 0.

**Kielelezo 7.1**



07 a) Viraguo, ni mofimu zinazo weza kukamili
sha maana ya neno katika lugha yaani huweza
kuwekwa mwanzo au mwisho wa mzizi wa
neno.
b) Vikwamizi, ni matatizo yanayo changia
kutofikia malengo fulani juu ya Jambo yanaweza
kuwa ya mazingira au mtu binafsi katika Jambo
c) Nazali, ni kiwango cha elimu cha
watoto wenye umri mdogo ambao husoma
au kupata maarifa kulingana na umri wao.
d) Viyeyusho, ni vitu vinavyo fanya
Jambo kitu kuyeyuka mfano jua, moto
au maji.

**Kielelezo 7.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutumia mifano kueleza maana ya dhana zilizoulizwa kutokana na kukosa uelewa juu ya mada ya *Matamshi na Lafudhi ya Kiswahili.*

Asilimia 3.3 ya watahiniwa walipata alama za wastani ambazo ni kuanzia 2 hadi 2.5 kwa kuwa walijaribu kutoa maana ambazo si toshelevu. Baadhi yao waliweza kutoa mifano sahihi ya sauti za Kiswahili katika dhana lakini walishindwa kueleza maana ya dhana hizo. Wengine waliweza kutoa maana sahihi huku wakishindwa kutoa mifano sahihi ya sauti za Lugha ya Kiswahili.

Vilevile, watahiniwa wachache ambao ni asilimia 2.2 ya watahiniwa wote waliojibu swali hili walifanikiwa kupata alama za juu kuanzia 3 hadi 4. Mathalani, kuna mtahiniwa mmoja tu kati ya watahiniwa wote waliojibu swali hili ambaye aliweza kupata alama zote 4. Huyu aliweza kutoa maana sahihi na mifano sahihi kwa dhana zote zilizoulizwa katika vipengele vyote vya swali. Mtahiniwa huyu anaonekana anaimudu vizuri mada hii. Kielelezo 7.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama 4.

**Kielelezo 7.2**


07 (a) Vipasuo

Ni konsonanti (sauti) ambazo hutolewa na binadamu ambapo ala za sauti huwa zimefunga mkondo wa hewa na kuachia kwa ghafla kuruhusu mkondo wa hewa kupita. p, b, t, d.

(b) Vikwamizi

Ni konsonanti ambazo hutamkwa wakati ala za sauti ~~zimefunga kabisa mkondo wa hewa~~ Sauti zilizokuwa zimefunga kwania mkondo wa hewa zikiachia

(c) Nazali

Ni konsonanti ambazo hutamkwa huku hewa ikitoka kwenye mapafu ikipita puani kutokana na kufungwa kwa ala za sauti katika pango hewa. n, ng, ŋ

(d) Viyeyusho

Ni konsonanti zinazotamkwa pasipo mkatano wowote wa ala za sauti / mzuio wowote wa ala za sauti. y, w.

(e) Vikwamizi

Ni konsonanti ambazo hutamkwa huku ala za sauti zikiwa zimekaribiana sana na kuacha upenyo mwembamba sana wa hewa kupita. f, v, z, s, θ


**Kielelezo 7.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kutoa maana ya dhana za kifonolojia na kuweka mifano sahihi kwa kila dhana.

### 1.1.8 Swali la 8: Maendeleo ya Kiswahili

Swali hili lilitoka katika mada za Kitaaluma hususan mada kuu ya *Maendeleo ya Kiswahili*. Mtahiniwa alitakiwa kuainisha kazi nne za iliyokuwa Kamati ya Lugha ya Nchi za Afrika Mashariki katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 4.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 98.7 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu na ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Asilimia 87.6 ya


watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama za wastani na zaidi. Chati namba 8 inafafanua viwango vya kufaulu kwa asilimia.




**Chati Namba 8**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 57.5 ya watahiniwa waliojibu swali hili walijibu swali hili vizuri. Watahiniwa hawa walipata alama za juu kuanzia 3 hadi 4. Baadhi yao waliweza kuainisha kazi zote nne za iliyokuwa Kamati ya Lugha ya Nchi za Afrika Mashariki katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili kwa sababu walielewa vizuri mada ya Maendeleo ya Kiswahili na matakwa ya swali. Kwa mfano, kazi nne za iliyokuwa Kamati ya Lugha ya Nchi za Afrika Mashariki katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili zilizoainishwa na watahiniwa wa kundi hili ni *kuhakikisha Kiswahili kinatumika kama chombo cha mawasiliano, kufanya Kiswahili kitumike katika vyombo vya habari, kufanya Kiswahili kuwa somo na kutafsiri vitabu vya kiingereza kwa Kiswahili*. Kielelezo 8.1 ni sampuli ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama 4.

**Kielelezo 8.1**



8. i. Kuhakikisha kiswahili kinatumika kama chombo cha mawasiliano
ii. Kukifanya kiswahili kitumike katika vyombo vya habari.
iii. Kuhakikisha kiswahili kinatumiwa katika mikutano ya nchi
iv. Kukifanya Kiswahili kuwa ni mingo ni mwa somo katika Shule zote za Afrika mashariki

**Kielelezo 8.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuainisha kazi nne za iliyokuwa Kamati ya Lugha ya Nchi za Afrika Mashariki katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili.

Vilevile, asilimia 30.1 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama za wastani kunzia 2 hadi 2.5. Watahiniwa hawa hawakujibu swali hili kikamilifu kwa sababu anuwai. Mathalani, baadhi yao waliweza kuonesha kazi mbili za iliyokuwa Kamati ya Lugha ya Nchi za Afrika Mashariki huku wengine wakitoa maelezo yasiyojitosheleza kikamilifu.

Hata hivyo, kuna asilimia 12.4 ya watahiniwa ambao walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5 kutokana na kutokuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, baadhi yao walitoa majibu ambayo yanaeleza nyenzo zilizotumika katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili ambazo ni vyombo vya habari, biashara, dini na utawala badala ya kuainisha kazi nne za iliyokuwa Kamati ya Lugha ya Nchi za Afrika Mashariki (*kuhakikisha Kiswahili kinatumika kama chombo cha mawasiliano*, *kufanya Kiswahili kitumike katika vyombo vya habari*, *kufanya Kiswahili kuwa somo na kutafsiri vitabu vya kiingereza kwa Kiswahili*). Kielelezo 8.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili vizuri na kupata alama 0.

**Kielelezo 8.2**



8. i/ Vyombo vya habari
ii/ Biashara
iii/ Utawala
iv/ Dini

**Kielelezo 8.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeainisha nyenzo zilizotumika katika kukuza na kueneza Kiswahili badala ya kuainisha kazi nne za iliyokuwa Kamati ya Lugha ya Nchi za Afrika Mashariki katika kukuza na kueneza Kiswahili.

### 1.1.9 Swali la 9: Upimaji

Swali hili lilitoka katika mada za Kitaalamu hususan mada kuu ya *Upimaji*. Swali lilimtaka mtahiniwa abainishe mambo manne ambayo mwalimu anapaswa kuyazingatia ndani ya chumba cha mtihani. Aidha, swali hili lilikuwa na jumla ya alama 4.


Asilimia 99.7 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walijibu swali hili na lilikuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Asilimia 96.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani na zaidi. Chati namba 9 inafafanua viwango vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Namba 9:** Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 82.7 ya watahiniwa walijibu vizuri swali hili kwa kuzingatia matakwa ya swali. Kati yao, kuna walioweza kubainisha mambo manne ambayo mwalimu anapaswa kuyazingatia katika chumba cha mtihani ambayo ni *kusimamia mtihani kwa haki, kuchukua orodha ya wanafunzi waliofanya mtihani, kusikiliza shida za wanafunzi na kuzitatua na kuhakikisha hakuna udanganyifu*. Hii inaonesha kwamba watahiniwa hawa wanaimudu mada ya *Upimaji* na walielewa vizuri matakwa ya swali. Kielelezo 9.1 ni majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri na kupata alama 4.

**Kielelezo 9.1**





**Kielelezo 9.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kubainisha mambo manne ambayo mwalimu anapaswa kuyazingatia katika chumba cha mtihani.

Asilimia 13.5 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5 kwa kuwa majibu yao hayakujitosheleza. Baadhi yao walibainisha mambo mawili badala ya mambo manne kama swali lilivyotaka huku wengine wakishindwa kutoa maelezo sahihi juu ya mambo waliyobainisha.

Aidha, asilimia 3.8 walipata alama hafifu ambazo ni kuanzia 0 hadi 1.5. Baadhi yao hawakuelewa matakwa ya swali na wengine hawakuwa na uelewa wa kutosha katika mada hii. Mathalani, baadhi yao walijibu mambo ambayo mtu anaweza kuyazingatia mahali popote na kwa shughuli yoyote badala ya kubainisha mambo ambayo mwalimu anapaswa kuyazingatia katika chumba cha mtihani. Kielelezo 9.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuelewa matakwa ya swali na kupata alama 0.

**Kielelezo 9.2**




9. i/ Utulivu au usikivu.
ii/ Muda.
iii/ Mawasiliano.
iv/ Idadi ya wanafunzi.

**Kielelezo 9.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume cha matakwa ya swali.

### 1.1.10 Swali la 10: Upimaji

Swali hili lilitoka katika mada za Kitaalamu hususan katika mada kuu ya *Upimaji*. Swali lilihitaji mtahiniwa achambue mbinu nne ambazo mwalimu hutumia kufanya tathmini ya somo darasani. Swali lilikuwa na jumla ya alama 4.


Asilimia 99.1 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walijibu swali hili na ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vibaya kwa kuwa asilimia 68.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu. Chati namba 10 inafafanua viwango vya kufaulu kwa asilimia.




**Chati Namba 10**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Aidha, watahiniwa wengi ambao ni asilimia 68.4 ya waliojibu swali hili walipata alama hafifu ambazo ni kuanzia 0 hadi 1.5 kwa kuwa hawakuelewa matakwa ya swali. Vilevile, baadhi yao hawakuwa na uelewa juu ya mada ya *Upimaji*. Kwa mfano, wengine waliorodhesha aina za tathmini ambazo ni *tathmini awali, tathmini endelevu, tathmini tatuzi na tatmini tamati* badala ya kuchambua mbinu nne ambazo mwalimu anaweza kuzitumia kufanya tathmini kama vile *kuangalia mafanikio ya malengo mahsusi, zana zilizotumika kufundishia, mbinu na kupitia maoni ya wanafunzi*. Kielelezo 10.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu aina za tathmini badala ya mbinu za kufanya tathmini ya somo darasani na kupata alama 0.

**Kielelezo 10.1**


10 (i) Tathmini awali, Hii ni mbinu anayotumia Mwalimu katika kufanya tathmini darasani ambayo mwalimu anatumia mwanzoni mwa kipindi kupima uelewa wa wanafunzi au kubaini maarifa aliyonayo mwanafunzi,

(ii) Tathmini endelevu, Hii ni mbinu anayoitumia mwalimu kufanya tathmini ya somo darasani ambayo inakuwa ni endelevu katika kupima maendeleo ya mwanafunzi,

(iii) Tathmini tafuzi, Hii ni mbinu anayotumia mwalimu kufanya tathmini ya somo darasani katika kubaini ugumu na matatizo ya wanafunzi katika kujifunza na kuyatatua matatizo hayo,

(iv) Tathmini tamati, Hii ni mbinu inayo fanyika mwishoni mwa kipindi au Mwanafunzi amalizapo shule,

**Kielelezo 10.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeorodhesha aina za tathmini badala ya kuchambua mbinu ambazo mwalimu anaweza kuzitumia kufanya tathmini darasani.

Vilevile, asilimia 22.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifanikiwa kuchambua vizuri mbinu mbili tu na hivyo kupata alama za wastani ambazo ni kuanzia 2 hadi 2.5. Baadhi yao walichambua mbinu mbili kwa ufasaha badala ya mbinu nne ambazo mwalimu anaweza kuzitumia kufanya tathmini darasani. Aidha, wengine waliweza kuorodhesha mbinu nne huku wakishindwa kuzichambua kwa usahihi.

Asilimia 9.5 ya watahiniwa waliojibu swali hili walijibu vizuri, kwa sababu walielewa vizuri matakwa ya swali. Hawa waliweza kuchambua mbinu nne atakazotumia mwalimu kufanya tathmini ya somo darasani ambazo ni *kuangalia mafanikio ya malengo mahsusi, zana zilizotumika kufundishia, mbinu na kupitia maoni ya wanafunzi*. Kielelezo 10.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama 4.

**Kielelezo 10.2**

| | |
|---|---|
| 10. | Mbinu atakazotumia Mwalimu kufanya tathmini ~~ndani~~ ya Somo Darasani. |
| i. | Kwa kuangalia Majaribio ya Malengo Mahususi aliyoyaandika ndani ya darasa. Mbinu hii ni kuweza kugundua jee amefikia kwa kiwango gani Malengo Mahususi. |
| ii. | Kwa kuangalia Zana ya kufundishia aliyoitumia. Jee zana aliyoitumia inamuwezesha Mwanafunzi kweli kuelewa kwa haraka, jee Zana imesawili na Lengo Mahususi nitakapokuwa nikipitia Zana anaweza kufanya tathmini. |
| iii. | Kwa kuangalia Mbinu ya ufundishaji iliyotumika. kwa namna ya kwamba Uteuzi Mzuri wa Mbinu huwa unasaidia uwasilishaji wa Maarifa kwa Mwanafunzi endapo Mbinu iliyotumika sio nzuri kwa Mwanafunzi ni vigumu kwa Lengo la kufikiwa kwa somo. |
| iv. | Kwa kupitia ~~Maono~~ Maoni ya wanafunzi ambayo yanaendana sambamba na ~~zoezi~~ Matokeo ya Zoezi lilitolewa mwishoni ~~baadaya~~ wa kipindi. Hii itasaidia Mwanafunzi kueleza ameelewa nini Somo na nini kimemshinda katika Somo na wapi hakuelewa Somo pia na Matokeo ya Zoezi huwa pia ni Miongoni mwa mbinu ya tathmini ya Somo darasani. |


**Kielelezo 10.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuchambua mbinu nne atakazotumia mwalimu kufanya tathmini ya somo darasani.

### 1.2 SEHEMU B: TAALUMA

#### 1.2.1 Swali la 11: Fasihi

Swali hili lilikuwa la insha na lilihusu mada ya *Fasihi*, hususan katika kipengele cha ushairi. Mtahiniwa alitakiwa kutunga shairi la kisasa na kisha alitumie kufafanua sifa nne za mashairi ya kisasa. Swali lilikuwa na jumla ya alama 15, ambapo kipengele cha kutunga shairi kilikuwa na alama 3 na kipengele cha kufafanua sifa nne za mashairi ya kisasa kilikuwa na alama 12.

Asilimia 94 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili na ni miongoni mwa maswali ambayo yalijibiwa vizuri. Asilimia 82.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani na zaidi. Chati namba 11 inafafanua viwango vya kufaulu kwa asilimia.




**Chati Namba 11**: Kufaulu kwa Watahiniwa katika Asilimia

Aidha, ilibainika kuwa asilimia 52.7 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za juu kuanzia 10.5 hadi 15. Wengi wao walielewa matakwa ya swali na hivyo waliweza kutunga shairi la kisasa kwa usahihi na kisha walilitumia kufafanua sifa nne za mashairi ya kisasa. Sifa zilizochambuliwa ni pamoja na *kutokufuata urari wa vina na mizani*, *mishororo kutokuwa na urari wa idadi ya mizani*, *hayana idadi maalum ya*

*mishororo katika ubeti , hayaimbiki na hayana kituo*. Kielelezo 11.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

**Kielelezo 11.1**

11. ELIMU

Sikiliza rafiki,
Ushauri ninakupa,
Japo wote tu sawa,
Ila ombi unisikilize.

Elimu ni jambo muhimu,
Kwa dunia ya sasa,
Hivyo yatupasa tuzingatie.


Ulimwengu umebadilika,
Mambo yameongezeka,
Yote yanahitaji elimu,
Ili tuweze kuyamudu,
Rafiki nakuomba,
Elimu zingatia.

Kwa kutumia shairi la hapo juu, zifuatazo ni sifa za mashairi ya kisasa.

Hayafuati urari wa vina na mizani. Vina ni silabi za mwisho katika kila mstari na mizani ni idadi ya silabi katika ubeti. Mashairi ya kisasa hayazingatii ufanano wa vina na mizani. Kwa mfano katika shairi hili katika ubeti wa kwanza kila mstari unaishia tofauti na mstari unaofuata. Pia kwa upande wa mizani kila mstari una idadi tofauti. Kwa mfano katika ubeti wa pili:

"Elimu ni jambo muhimu,
Kwa dunia ya sasa,
Hivyo yatupasa tuzingatie"

Mstari wa kwanza una jumla ya mizani tisa, wa pili mizani saba na wa tatu mizani kumi na moja.



11. Hayana idadi maalumu ya mistari katika beti. Tofauti na mashairi ya kimapokeo ambayo yanakuwa na idadi maalum ya mistari, mashairi ya kisasa hayana idadi maalum. Katika shairi hili, ubeti wa kwanza una mistari minne, ubeti wa pili una mistari mitatu na ubeti wa tatu una mistari sita.

Hayana kituo. Mashairi ya kisasa hayana mstari ambao hujirudia katika kila ubeti. Mara nyingi mashairi ya kisasa kila ubeti una mstari wake tofauti. Kwa mfano katika shairi hili katika ubeti wa kwanza ni "Ila ombi unisikilize", katika ubeti wa pili kituo ni "Hivyo yatupasa tuzingatie", na katika ubeti wa tatu kituo ni "Elimu zingatia". Hivyo mashairi ya kisasa kila kituo hutofautiana na ubeti mwingine.

Ni rahisi kuyaandaa. Mashairi ya kisasa hayachukui muda mwingi katika kuyaandaa tofauti na mashairi ya kimapokeo ambayo yanahitaji kufuata sheria na kanuni zote za uandishi wa mashairi. Katika kuandaa mashairi ya kisasa, mwandishi anahitaji kuwa na wazo ambalo atalitumia.

Hizi ni sifa za mashairi ya kisasa. Lakini pia, mashairi ya kisasa yana umuhimu sawa wa mashairi ya kimapokeo ambao ni kufikisha ujumbe kwa jamii.

**Kielelezo 11.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetunga vizuri shairi la kisasa na kisha kulitumia katika kufafanua sifa nne za mashairi ya kisasa kwa ufasaha.

Aidha, kuna watahiniwa ambao walipata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10. Hawa walikuwa ni asilimia 30.1 ya watahiniwa wote waliofanya swali hili. Wengi wao walishindwa kuhusisha mashairi waliyotunga na sifa za

mashairi ya kisasa. Aidha, wengine walitunga shairi la kimapokeo huku wakifafanua sifa za mashairi ya kisasa.

Hali kadhalika, watahiniwa wachache ambao ni asilimia 17.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 5.5. Hii inaonesha hawakuelewa matakwa ya swali na wengine walikosa uelewa juu ya mada ya *Fasihi*. Baadhi yao walishindwa kutunga shairi la kisasa. Aidha, wengine walitunga shairi la kimapokeo na kutaja sifa za mashairi ya kimapokeo badala ya sifa za mashairi ya kisasa kinyume cha matakwa ya swali. Kielelezo 11.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili vibaya na kupata alama hafifu.

**Kielelezo 11.2**

11. Ushairi ni utungo unaoandaliwa kwa ajili ya kuimbwa. Lifuatalo ni shairi la kisasa.

HONGERA MAMA

1. Hongera kwako mama, yalomema kunipatia,
Haukusita kuyasema, mazuri kuzingatia,
Nilipokua ulisimama, huduma kunipatia,
Hakika mama nakupenda, Na Mola akujalie.

2. Hukupenda kuniacha, peke yangu chumbani,
Kifuani ulinificha, nisiangamie hasirani,
Kunibeba hukuacha, nibunidike mgongoni,
Hakika mama nakupenda, Na mola akujalie.

3. Wewe ni Mama mwema, hakika unaweza,
Matendo yako ni mema, hakika unaweza,
Nitakujali kwa wema, kwa kuniwezesha,
Hakika mama Nakupenda, Na mola akujalie.

Sifa


i Lazima lizingatie urari wa mizani
ii Liwe linaimbika
iii Liwe na vina vinavyofanana
iv Liwe na kibwagizo.

**Kielelezo 11.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetunga na kutaja sifa za mashairi ya kimapokeo badala ya kutunga na kueleza sifa za mashairi ya kisasa.

### 1.2.2 Swali la 12: Uhakiki wa Kazi za Fasihi

Swali hili lilikuwa la insha na lilihusu mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*, hususan kipengele cha tamthiliya. Mtahiniwa alitakiwa kuthibitisha kuwa mmomonyoko wa maadili ni miongoni mwa changamoto inayoikabili jamii. Katika kuthibitisha kauli hiyo, mtahiniwa alitakiwa kutumia tamthiliya ya MWALIMU ROSE iliyoandikwa na *Ambrose F. Mghanga*. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 15 ambapo mtahiniwa alitakiwa atoe hoja tano kuthibitisha kauli hiyo. Kila hoja iliyotolewa ilikuwa na uzito wa alama 2½ huku utangulizi wa insha ukiwa na uzito wa alama 1½ na hitimisho la insha likiwa na uzito wa alama 1.

Asilimia 91.7 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili na ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Asilimia 99.6 ya watahiniwa walipata alama za wastani na zaidi. Chati namba 12 inafafanua viwango vya kufaulu kwa asilimia.




**Chati Namba 12:** Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 79.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za juu kuanzia 10.5 hadi 15. Wengi wao walielewa matakwa ya swali na hivyo wakaweza kuchambua tamthiliya ya MWALIMU ROSE kwa kuibua mambo ambayo yanadhihirisha mmomonyoko wa maadili unavyoikabili

jamii. Mambo yaliyoibuliwa na watahiniwa wa kundi hili ni kama vile *uongozi mbaya, ulevi, uasherati uliosababisha maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi, imani potofu na dharau*.Kielelezo 12.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili kwa kueleza mambo ambayo yanathibitisha kuwapo kwa mmomonyoko wa maadili katika jamii na kupata alama za juu.

**Kielelezo 12.1**

12. Mmomonyoko wa madili ni kitendo cha kuwa
na tabia mbaya ambazo hazistahili katika jamii.
Mmomonyoko wa maddili ~~siyo~~ sio kwa vijana au
watoto tu bali na watu wazima pamoja
na viongozi wa hali ya juu huwa na mmomonyo-
ko wa maadili. Kwa kutumia tamthiliya ya
MWALIMU ROSE iliyoandikwa na Ambrose F
Mghanga. Kuthibitisha kwa hoja tano kuwa
mmomonyoko wa maadili ni miongoni mwa changa-
moto inayokabili jamii:-

Uongozi mbaya; Ugonzi mbaya umejitokeza
katika ~~riwaya~~ tamthiliya ya mwalimu Rose ambayo
inasababisha mmomonyoko wa maadili katika
jamii. Hapa tunamuona Afisa Elimu Bwana Majaliwa
alitumia uongozi wake na cheo chake katika
kuwaongoza watu vibaya kwa kuwanyanganya
walimu haki zao za msingi kama mshahara
wa mume wa mwalimu Rose na pia alitumia
cheo chake kutembea na wanafunzi pamoja na
walimu wa kike. Kwahiyo uongozi mbaya ni moja
wapo ya mmomonyoko wa maadili katika jamii.

Ulevi; Ulevi ni miongoni mwa mmomonyo-
ko wa maadili katika jamii. Katika tamthiliya
hii ya Mwalimu Rose tunamuona Mwalimu
Rose aliyekuwa akitembea na Afisa elimu aliku-
wa akilewa na kurudi nyumbani kwa mume
wake akiwa amelewa na kuanza kutukana tuka-
na ovyo na mbaya zaidi alikuwa akimtukana
mume wake pamoja na watoto wake.
Katika jamii zetu za sasa watu wengi wana-
kunywa sana pombe mpaka wanalewa na pia
wanashindwa kuzihudumia familia zao kwasababu

12. ya kunywa pombe. Pia katika jamii zetu watu wakilewa wanaanza kutukana kuongea matusi ambayo hayastahili katika jamii jambo ambalo linasababisha mmomonyoko wa maadili katika jamii zetu.

Ugonjwa wa Ukimwi; ugonjwa wa Ukimwi ni ugonjwa unaosababishwa na mmomonyoko wa maadili katika jamii. Kwa kuthibitisha kauli hii kupitia kitabu cha Mwalimu Rose tunamuona mwalimu Rose alivyo pata ugonjwa wa ukimwi kutokana na uasherati pia hata bwana Majaliwa alipata ugonjwa wa ukimwi kutokana na kutembea na wanawake wengi pamoja na wanafunzi wake kwasababu ya cheo chake alicho kuwa nacho. Hapa tunamuona Mwalimu Rose alivyofanya tendo la ndoa na Bwana Majaliwa bila kutumia kondomu na kupata ugonjwa wa Ukimwi. Pia katika jamii zetu kuna watu wanaoishi na virusi vya ukimwi kutokana na umalaya na uasherati wanaoufanya. Pia hapa tunamuona Bwana Majaliwa alipoanza kudhoofu na kupelekwa hospitalini kupima na kukutwa ana ugonjwa wa ukimwi.

Imani potofu; Imani potofu ni fikra mbaya anazokuwa nazo mtu kumshirikisha Mungu au Imani za kishirikina. Hapa tunamuona Mwalimu Rose na Bwana majaliwa wakienda kwa mganga ili aweze kuwanyanyashia nyota zao waweze kupandishwa cheo pia wapate hela nyingi ili waweze kufanya starehe! Pia katika jamii za sasa watu wengi wanatafuta vyeo

12. Kufanya mambo ya ushrikina ili waweze kupata pesa nyingi na kuwa matajiri.

Dharau; Hiki ni kitendo cha kuto-muheshimu mtu. Na katika tamthiliya hii ya Mwalimu Rose, tumemuona Mwalimu Rose alivyokuwa anamdharau mume wake Bwana Makoma kwa kutofika nyumbani kwa wakati na anapofika nyumbani na kumkuta mume wake Mwalimu Rose anaa-nza kumtukana mume wake. Pia Mwalimu Rose alikuwa akiondoka nyumbani na kulala nje ya ndoa yake bila kumuaga mume wake. Kwahiyo dharau ni sehemu moja wapo ya mmomonyoko wa maadili katika jamii jambo ambalo ni changamoto katika jamii. Na katika jamii zetu ni jambo ambalo lina fanywa na wanawake wengi. Wanawake wanawadharau wanaume wao kwa kutowajali na kuwothamini katika ndoa zao.

Kwa kuhitimisha; Mmomonyoko wa maadili unasababishwa na wazazi wote wawili baba na mama ndo maana hata watoto unakuta wanakuwa na tabia mbaya katika jamii na hizo tabia wanaiga kutoka kwa wazazi wao. Kwahiyo ningependa wazazi wawalee vizuri watoto wao katika maadili bila kuonyesha tofauti zao mbele ya watoto wao ili kuweza kuziepuka changamoto za mmomonyoko wa maadili katika jamii.

**Kielelezo 12.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri kwa kuibua mambo ambayo yanadhihirisha namna suala la mmomonyoko wa maadili linavyoikabili jamii kwa kutumia tamthiliya ya MWALIMU ROSE.

Aidha, kulikuwa na watahiniwa ambao walipata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10. Hawa walikuwa asilimia 20 ya watahiniwa wote waliojibu swali hili. Wengi wao hawakufafanua kikamilifu mambo yaliyomo katika tamthiliya ya MWALIMU ROSE ambayo yanadhihirisha kuwapo kwa mmomonyoko wa maadili katika jamii.

Hali kadhalika, asilimia 0.4 pekee ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 5.5. Baadhi yao hawakuelewa matakwa ya swali na wengine hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada hii. Kutokana na hali hiyo kuna baadhi ya watahiniwa ambao hawakuweza kueleza hoja tano zinazodhihirisha kuwapo kwa mmomonyoko wa maadili katika jamii na badala yake walieleza hoja tatu au pungufu ya hizo. Kielelezo 12.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kufafanua hoja zote tano kikamilifu na kupata alama hafifu.

**Kielelezo 12.2**

12 Mwalimu Rose; ni Tamthiliya iliyo andikwa na Mwandishi Ambrose F. - Mghanga na Inajadili baadhi ya changamoto ambazo zinaikabili jamii ambazo ni kama Ulevi lakini za Kishirikina. Usaliti nakadhalika. hivyo "Mmomonyoko wa Maadili ni Miongoni mwa Changamoto inayokabili jamii" Hivyo kutokana na hoja hii tamthiliya ya Mwalimu Rose Imeeleza changamoto zingine zinazosababisha - Mmomonyoko wa Maadili.

Suala la Malezi Mabaya kwa - watoto; Mfano Mwalimu Rose hakuwa na Malezi Mazuri kwa wanae kwani alikuwa na Mambo Mengi kiasi cha kukosa Muda wa kukaa na wanae na kuwafundisha Malezi Mazuri.

Mapenzi na ndoa; Mfano Mwalimu Rose alikuwa akitembea na wengine hali akiwa na Mumewe hivyo hii pia husababisha na mmomonyoko wa Maadili katika k jamii. na pia Mwalimu Rose alikuwa akitoka nje ya ndoa yake.


Suala la Ulevi; Hii pia ni jambo ambalo husababisha Mmomonyoko wa Maadili katika jamii mfano. Mwalimu Rose pia alikuwa Mlevi na kutokana na Ulevi Mtu - yeyote anaweza kuongea au kufanya na hata mbele za watu hivyo ni changamoto katika jamii.

**Kielelezo 12.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu kwa sababu alieleza hoja tatu pekee zinazodhihirisha kuwapo kwa mambo yanaosababisha mmomonyoko wa maadili katika jamii.

### 1.2.3 Swali la 13: Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili

Swali hili lilikuwa la insha na lilihusu mada ya *Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili*, hususan kipengele cha uundaji wa maneno. Mtahiniwa alitakiwa kutumia mifano kubainisha njia tano zinazoweza kutumika katika uundaji wa maneno. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 15 ambapo mtahiniwa alitakiwa abainishe hoja tano. Kila hoja iliyotolewa ilikuwa na uzito wa alama 2½ huku utangulizi wa insha ukiwa na uzito wa alama 1½ na hitimisho alama 1.

Asilimia 94 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili na ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Asilimia 100 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani na zaidi. Chati namba 13 inafafanua viwango vya kufaulu katika asilimia.




**Chati Namba 13:** Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 89 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za juu kuanzia 10.5 hadi 15. Hawa waliweza kubainisha njia tano za uundaji wa maneno kwa ufasaha huku wakitoa mifano sahihi kutoka katika lugha ya Kiswahili. Njia zilizobainishwa ni pamoja na *uambishaji, njia ya kutohoa, urudufishaji, mwambatano, tanakali sauti, mwigo wa maumbo ya vitu na uakronimishaji.*Watahiniwa hawa walielewa kikamilifu mada ya *Utumizi*

*wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili*, hususan kipengele cha uundaji wa maneno. Kielelezo 13.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.

**Kielelezo 13.1**

13. Uundaji wa maneno ni namna
maneno yanavyoweza kuundwa
au kutokea aina kuzaliwa, kuna
njia mbalimbali zinazoweza kutu
mika kuunda maneno katika
lugha ya Kiswahili. Zifuatazo
ni njia za kuunda Maneno
i) Uambishi hii ni njia ambayo
inatumika kuunda maneno.
au aina za maneno mbalimbali

13 Katika Lugha ya Kiswahili kwa kuweka viambishi awali au tamati mwanzoni na ~~ah~~ mwishoni mwa neno au mzizi wa neno au shina

Mfano
i) Lima — Kilimo
— Mkulima

ii) Taifa — Taifisha
Hivyo basi asili ya neno hubaki asilika na kuzaliwa neno lingine kabisa.

ii) Pia njia ya kutohoa. Hii ni njia ya kuunda maneno kwa njia ya kuchukua neno kutoka lugha nyingine kuweka katika lugha ya Kiswahili Mfano wa maneno yaliyotoholewa kutoka lugha ya Kingereza ni kama vile
~~Shat~~

| Kiswahili | Kingereza. |
|---|---|
| i) Shati | — Shirt |
| ii) Skati | — Skirt. |

Hivyo njia hiyo tunapata msamiati mpya wa lugha ya Kiswahili na kutumika katika mawasiliano

iii) Urudufishaji. Hii ni njia ya kuunda maneno. Njia hii hutokea kwa kurudiarudia maneno na kuunda neno

13 moja au msamiati mmoja wa lugha ya Kiswahili.
Mfano harakaharaka.
neno hilo limetokana na kudia rudia kwa neno na kupata neno moja.
iv) Mwambatano. Njia hii pia ni njia ambayo hutumia kuunda au kupata msamiati mpya wa Kiswahili kwa kuambatanisha maneno mawili tofauti na kupata neno moja
Mfano neno Mwana na hewa tunapata neno moja ambalo ni Mwanahewa
Hivyo kupitia njia hiyo msamiati mpya au neno jipya hutokea.
v) Tanakari Sauti. Hii pia ni njia ambayo huunda neno au msamiati katika lugha na kuweza neno jipya kutokea kwa kufuata mlio au mwingo wa sauti ya kitu
Mfano neno pikipiki limetokana na kifaa chenyewe kinavyotoa sauti kikiwa kwenye matumizi yake.
Msamiati au maneno huundwa kwa njia hizo na kupitia hizo njia tunakuza lugha na kuongezeka kwa misamiati katika lugha.

**Kielelezo 13.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyebainisha njia tano za uundaji wa maneno kwa ufasaha na kutoa mifano sahihi kwa kila njia.

Aidha, kulikuwa na watahiniwa ambao walipata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10. Hawa walikuwa asilimia 11 ya watahiniwa wote waliojibu swali hili. Baadhi yao waliweza kubainisha njia za uundaji wa maneno ingawa hawakutoa mifano sahihi. Wengine walibainisha njia nne badala ya tano kama yalivyokuwa matakwa ya swali na kushindwa kutoa maelezo ya kila njia kikamilifu.


Hili ndilo swali lililojibiwa vizuri na watahiniwa wengi kuliko maswali yote katika mtihani huu, kwani hakukuwa na mtahiniwa aliyepata alama hafifu katika swali hili. Watahiniwa wote walipata alama za wastani na zaidi. Hii inaonesha kuwa kipengele cha uundaji wa maneno kilifunzwa na kueleweka vizuri na watahiniwa wengi.

## 1.3 SEHEMU C: UTAALAMU

### 1.3.1 Swali la 14: Zana za Kujifunzia na Kufundishia Somo la Kiswahili

Swali hili lilikuwa la insha na lilihusu mada ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia somo la Kiswahili*, hususan kipengele cha uandaaji wa zana hizo. Mtahiniwa alitakiwa kueleza tofauti tano zilizopo kati ya zana halisi na zana bandia. Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 15. Kila hoja ilikuwa na uzito wa alama 2½ huku utangulizi wa insha ukiwa na uzito wa alama 1½ na hitimisho alama 1.

Asilimia 64.3 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu walijibu swali hili na lilikuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Asilimia 88.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani na zaidi. Chati namba 14 inafafanua viwango vya kufaulu kwa asilimia.




**Chati Namba 14:** Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Asilimia 36.1 walijibu swali hili vizuri kwa viwango tofauti na kupata alama kuanzia 10.5 hadi 15. Hawa waliweza kuelewa matakwa ya swali na walikuwa na uelewa juu ya mada ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia somo la Kiswahili,* kwa sababu waliweza kueleza tofauti tano zilizopo kati ya zana halisi na zana bandia huku wakitoa mifano sahihi. Kielelezo 14.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa  aliyeweza kueleza kwa ufasaha tofauti tano zilizopo kati ya zana halisi na zana bandia ingawa hakuonesha utangulizi kwenye insha yake.


**Kielelezo 14.1**

14 Tofauti zilizopo kati ya zana halisi na zana
bandia ni hizi zifuatazo:-
Zana halisi hazina gharama wakati
zana bandia zina gharama. Kwa mfano
kwa kutumia zana halisi mwalimu ana-
weza akachukua kitu chochote kutoka kati-
ka mazingira yake na akaweza kufundi-
shia ilimradi tu iendane na somo husika.
kama mwalimu wa somo la geografia anawe-
za akawatoa wanafunzi wake nje na aka-
wafundisha aina za udongo kupitia udo-
ngo uliopo nje au mwalimu akauchimba
akaja nao darasani. Hii ni tofauti kwa
zana bandia ni lazima mwalimu aingie
gharama ya muda pia pesa ili kukami-
lisha zana yake.
Zana halisi humsaidia mwanafunzi
akafanya mazoezi kwa uhalisi akiwa
nyumbani tofauti na zana za bandia.
Kwa mfano Mwalimu wa sayansi anaweza
akafundisha somo kuhusu namna mmea
unapojitengenezea chakula chake. Hii humsai-
dia mwanafunzi akayatumia yale mawazo
ya mwalimu kufanya mazoezi zaidi akiwa
nyumbani kwa uhalisi kabisa. Tofauti
na zana za bandia ambazo zitamchukua
a mwanafunzi muda mrefu kuweza kufa-
nya mazoezi akiwa peke yake.
Zana halisi hupatikana katika ma-
zingira yanayotuzunguka tena kwa muda
wowote tofauti na zana bandia zinazo
hitaji maandalizi ili kuweza kuzipata.

14 Zana halisi kama mimea, mawe, upepo na nyinginezo hupatikana bila kutumia nguvu nyingi yaani mwalimu huchagua tu kuli-ngana na hitaji lake. Lakini zana bandia mwalimu lazima afanye maandalizi kama ni manira, rangi, penseli na vitu vingine kama atahitaji zana ya kuchora. Hivyo zana halisi humrahisishia kazi mwalimu katika suala zima la ufundishaji na ujifunza-ji darasani.

Zana bandia zinahitaji ujuzi na ubunifu sana katika kuziandaa tofauti na zana za halisi. Hii ni kwa sababu inahusisha vitu vingi katika maandalizi ambayo vitamfanya mwalimu atengeneze zana zitakazo sawiri kitu halisi anachokwenda kukielezea. Tofauti na zana halisi ambapo mwalimu anaangalia tu mada na kuangalia katika mazingira tu kitu kinachofanana katika kuelezea somo hilo. Kwa mfano somo la hali ya hewa. Mwalimu anaweza akaangalia uelekeo wa upepo, mawingu, joto au mvua na akaweza kuelezea somo lake.

Zana halisi ni rahisi sana katika kuelezea somo kuliko zana bandia. Hii ni kwa sababu, mwanafunzi huelewa zaidi kupitia zana lakini zana halisi ni rahisi zaidi kwa sababu mwanafunzi anazio na kila siku katika mazingira yanayomzunguka. Kwa mfano somo la mmomonyoko wa udongo, mwanafunzi huona-



14. kila siku shuleni, nyumbani hata njiani
anapopita tofauti na zana za bandia
ambazo huwasilishwa kwa kuchorwa
na kupelekea mwanafunzi kuchukua
muda kidogo katika kuelewa.
Hivyo walimu wanashauriwa kama
kuna uwezekano wa kupatikana zana
halisi ambayo itaendana na somo la
siku hiyo, inatupasa tutumie ili kuweza
kujenga kumbukumbu ya muda mrefu na
uelewa mkubwa kwa wanafunzi. Na kama
hamna basi tutumie zana za bandia
ili kuweza kusaidia kueleza somo hilo.

**Kielelezo 14.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kueleza tofauti tano zilizopo kati ya zana halisi na zana bandia kwa usahihi.

Aidha, asilimia 52.7 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10 kutokana na kushindwa kufafanua vizuri baadhi ya hoja walizotoa. Licha ya hayo, wengine waliandika insha bila kufuata alama za uakifishaji na wengine walitoa hoja pungufu badala ya hoja tano kama yalivyokuwa matakwa ya swali.

Hata hivyo, kulikuwa na watahiniwa wachache asilimia 11.2 ambao walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 5.5. Baadhi ya watahiniwa katika kundi hili walishindwa kuelewa mahitaji ya swali. Hii ni kwa sababu walijibu hoja ambazo ni kinyume cha matakwa ya swali kwa kuwa hoja hizo hazikuweza kutofautisha zana halisi na zana bandia. Kwa mfano, kuna mtahiniwa aliyejibu, “Zana halisi ni bora kuliko zana bandia.” Kwa kawaida, kila zana inaweza kuwa bora au isiwe bora kulingana na mahitaji ya somo lenyewe. Kielelezo 14.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye hakuelewa mahitaji ya swali na kupata alama hafifu.

**Kielelezo 14.2**



14 Zana halisi huondoa umakini na mvuto kwa wanafunzi, lakini zana ya bandia huvutia sana na huleta usikivu mkubwa sana kwa wanafunzi wanapokuwa wanajifunza.

Zana halisi hupoteza ukweni fu lakini zana bandia huleta ubunifu kwa mwalimu na mwanafunzi pia, hali hii ni muhimu sana kwa mwanafunzi.

Zana halisi ni kitu halisi ambacho huweza kuumuliwa na huweza kumpumbaza mwanafunzi lakini zana bandia huweza kumuongezea uwezo wa kufikiri na ufaulu mkubwa.

Huondoa uwezo wa kufikiri kwa mwanafunzi lakini zana bandia huongeza uwezo wa kufikiri kwa mwanafunzi, hivyo huongeza ufaulu.


**Kielelezo 14.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali kinyume cha matakwa ya swali kwa kueleza hasara za kutumia zana halisi na maana ya zana halisi isiyo sahihi badala ya kueleza tofauti zilizopo kati ya zana halisi na zana bandia.

## 1.3.2 Swali la 15: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili

Swali lilihusu mada ya *Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili.* Mtahiniwa alihitajika kuchambua faida tatu na hasara tatu za kutumia mbinu ya matembezi ya galare katika kufundisha na kujifunza somo la Kiswahili. Swali lilikuwa la insha na lenye uzito wa alama 15. Mtahiniwa alitakiwa kutoa hoja sita ambapo kila hoja ilikuwa na alama 2. Aidha, utangulizi ulikuwa na alama 1½ huku hitimisho likiwa na alama 1½.

Asilimia 86.8 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Aidha, swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwani asilimia

99.6 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama za wastani na zaidi. Chati namba 15 inafafanua viwango vya kufaulu kwa asilimia.




**Chati Namba 15:** Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Vilevile, asilimia 56 ya watahiniwa waliofanya swali hili walijibu vizuri kwa viwango tofauti na kupata alama kuanzia 10.5 hadi 15. Watahiniwa hawa waliweza kuchambua faida tatu na hasara tatu za kutumia mbinu ya matembezi ya galare katika kufundisha na kujifunza somo la Kiswahili. Uwezo huo unadhihirisha kwamba watahiniwa hao, walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Mbinu za Kufundisha na Kujifunzia Somo la Kiswahili*. Kielelezo 15.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu kwa kuweza kuchambua faida tatu na hasara tatu za kutumia mbinu ya matembezi ya galare katika kufundisha na kujifunza somo la Kiswahili.

**Kielelezo 15.1**

15 Mbinu ya galeri ni mbinu ya kufundi-
shia ambayo wanafunzi hupangwa kati
ka makundi na kupewa mada ya kujadili
wakimaliza hubandika ukutani ambapo
ambo katika kila kikundi anabaki mmoja
atayewapokea wageni kutoka makundi
mengine na kuwaelekeza au kufafanu-
lia walichokijadili katika kundi lao.
mbinu hii ina faida na hasara yake
kwakuanza na faida ni kama zifuata-
tazo.
Huwasaidia wanafunzi kupata maari-
fa mapya kutoka kwa wenzao; katika
kutumia mbinu hii wanafunzi hujifunza
au kupata maarifa mengine kutoka kwa
wenzao ambayo wao hajayapata katika
kundi lao.
Huwezesha ushirikiano baina ya wana-
funzi na kuvahirisha suala nzima la.


15 ujifunzaji; huu ni ukweli usiopingika kwa
mba kwa kutumia mbinu hii wanafu-
LS. nzi wanapata ushirikiano wakutosha kati
ka shala nzima la ujifunzaji hivyo kufanya
ujifunzaji kuwa halisi na kueleweka.

Huwafanya wanafunzi kuwa waja-siri na kuwa wabunifu; kupitia mbinu hii wanafunzi wanapata ujasiri mbele ya wenzao hata wale ambao wanaona aibu kuzungumza na wenzao. lakini mbali na hapo pia wanakuwa wabu-nifu wa kubuni mbinu nyingine na kujifunzia.

Pamoja na faida tuliona pia kuna hasara ya kutumia mbinu ya mate-mbezi ya galare, Hasara hizo kama zifuatazo;

Hupoteza muda; katika kutumia mbinu hii wanafunzi pamoja na waali-mu hutumia muda mwingi katika kuji-funza jambo dogo kwani kukaa kwenye makundi kujadili na kuandika ukurasa ni muda mrefu sana ambao unatumika, hivyo kukwamisha shughuli zingine.

Isiposimamiwa vizuri wanafunzi wa-chache tu ndio wanaofanya mjadala na kunufaika; huu ni ukweli usiopingika kwani baadhi ya wanafunzi wakati wa kujadili huwa hawaongei wala kuchangi-a [illegible] muda wa kutembea wakifika-kwenye kikundi kingine hakilizi maswa-li hata kama hajaelewa hivyo kukwa-


15 swala nzima la kujifunza kufanya lengo mahususi lisifikiwe.
Humafanya baadhi ya wanafunzi kuchukia somo; mbinu hii humafanya wanafunzi kudharaulima na wenzao hasa wale ambao uelewa wao ni mchini kwani mbinu hii inaonesha madhaifu yao kinayokuchukia somo na kudharauliwa na wenzao.
Hitimisho; mbinu hii ni nzuri sana lakini ilime nzuri zaidi serikali ijenge shule za kutosha pamoja na majengo ya kutosha ili wanafunzi wawe wachache darasani kwani kuenye darasa la wanafunzi mia moja ni vigumu kutumia mbinu hii.

**Kielelezo 15.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuchambua faida tatu na hasara tatu za kutumia mbinu ya matembezi ya galare katika kufundisha na kujifunza somo la Kiswahili kwa usahihi.

Vilevile, asilimia 43.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili kwa viwango vyao tofauti walipata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10. Watahiniwa hao walipata alama za wastani kutokana na kushindwa kufafanua vizuri baadhi ya hoja walizotoa. Licha ya hayo, wengine hawakujibu swali hili kwa ukamilifu kama ilivyotakiwa.

Pia, kulikuwa na asilimia 0.4 ya watahiniwa ambao walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 5.5. Baadhi ya watahiniwa hawa walishindwa kuelewa mahitaji ya swali badala yake walijibu hoja za kipengele kimoja tu cha swali. Baadhi walijibu kipengele cha faida tu huku wengine wakijibu kipengele cha hasara pekee. Vilevile, wengine walitoa hoja ambazo hazina mashiko ya kutosha. Wengine walichanganya mbinu ya galare, changanyakete na mbinu ya ziara. Kielelezo 15.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu kwa sababu alichanganya faida na hasara za mbinu ya matembezi ya galare na faida na hasara za mbinu ya ziara.

Majibu aliyoyatoa yanahusu faida na hasara za kutumia mbinu ya ziara badala ya mbinu ya matembezi ya galare.

**Kielelezo 15.2**

15. Mbinu ya matembezi ya galare Ni mbinu
ya kufundisha na kujifunzia ambayo humshirikisha
mwanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji ambao
mwalimu na wanafunzi hutembelea sehemu mbali-
mbali kama Mapango ya zamani, Mbuga za wanyama
mistu kwa ajili ya kujifunza mambo mbalimbali
yanayoendana na maada husika. Zifuatazo ni faida
na hasara za kutumia mbinu hiyo.
Humsaidia mwanafunzi kujifunza mambo
mengi ya Darasani na ya nje ya darasa: kwa
mfano mazingira ya mbuga za wanyama, Namna
ya kushirikiana na watu, Raha ya kusafiri na
mengineyo.
Humsaidia mwanafunzi kujenga kumbuku
mbu ya kudumu; maana ameona na kushika
huyo Sio rahisi kupoteza alichojifunza kwa
Urahisi kama akiwa Darasani
Humsaidia mwanafunzi kuwa mdadisi:

15 mbinu ya matembezi hupelekea mwanafunzi kuwa
mdadisi kwa sababu amebadilisha mazingira
na ameona vitu mbalimbali ambavyo hajawahi
kuona akiwa Darasani.

Pia mbinu ya matembezi ina hasara zipatazo
katika ujifunzaji na ufundishaji:

Hupoteza wakati; mfano, Huhitaji muda
wa kutosha kumwandaa mwanafunzi kwa ajili
ya kuchangia pia kama matembezi ni ya mbali
na shule huchukua muda mrefu kufika
kwa ajili.

Pia haishirikishi wanafunzi wote; kwa
sababu kama mwanafunzi hata pata mchango
wa kuchangia hatashiriki katika ujifunzaji
maana baadhi ya matembezi hutumia wajiri
hivyo basi mwanafunzi lazima achangie kiasi
hata kidogo cha nauli.

Pia hutumia Gharama; mfano kulipia
nauli, chakula na malazi. Kama matembezi
ni ya mbali huhitaji hela ya kutosha
kwa ajili ya kujikimu.


Hivyo basi njia hii ina umuhimu wake
pia na hasara zake hivyo walimu
wanapochagua mbinu za kufundishia na
kujifunzia lazima waangalie sile zinazoshiriki-
sha wanafunzi wote.

**Kielelezo 15.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu kwa sababu alieleza faida na hasara za kutumia mbinu ya ziara badala ya mbinu ya matembezi ya galare.

### 1.3.3 Swali la 16: Ufundishaji wa Mada Teule za Somo la Kiswahili

Swali hili lilihusu mada ya *Ufundishaji wa Mada Teule za Somo la Kiswahili*. Mtahiniwa alitakiwa kubainisha hatua tano zinazotakiwa kufuatwa katika kufundisha mada ya *Fasihi* kwa wanafunzi wa Kidato cha Kwanza. Swali lilikuwa la insha na lilikuwa na uzito wa alama 15. Mtahiniwa alitakiwa kubainisha hatua tano ambapo kila hatua ilituzwa alama 2½. Ili kupata jumla ya alama 15, utangulizi wa insha ulikuwa na alama 1½ ilihali hitimisho lilikuwa na alama 1.

Asilimia 48.9 ya watahiniwa waliofanya mtihani walijibu swali hili. Aidha, swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwa sababu asilimia 71.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani na zaidi. Chati namba 16 inaonesha viwango vya kufaulu kwa asilimia.




**Chati Namba 16**: Kufaulu kwa Watahiniwa kwa Asilimia

Aidha, watahiniwa wengine walipata alama za wastani kuanzia 6 hadi 10. Hawa walikuwa asilimia 50.7 ya watahiniwa wote waliofanya swali hili. Watahiniwa hao waliweza kubainisha hatua chache huku wengine wakishindwa kutoa maelezo yanayodhihirisha hatua walizotaja. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa waliweza kutaja hatua ya kukazia maarifa lakini wakashindwa kueleza kinachofanyika katika hatua hiyo.

Asilimia 20.5 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za juu kuanzia 10.5 hadi 15. Watahiniwa hawa walielewa matakwa ya swali na walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Ufundishaji wa Mada Teule za Somo la Kiswahili.* Baadhi yao waliweza kubainisha kikamilifu hatua tano zinazotakiwa kufuatwa katika kufundisha mada ya *Fasihi* kwa wanafunzi wa Kidato cha Kwanza. Kielelezo 16.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kubainisha hatua tano zinazotakiwa kufuatwa katika kufundisha mada ya *Fasihi* kwa wanafunzi Kidato cha Kwanza na kupata alama za juu.


**Kielelezo 16.1**

16. Hatua ni mtiririko anaoufuata mwalimu wa kati wa ufundishaji akiwa darasani. Hatua hizo husaidia mwalimu afundishe vizuri pale awapo darasani. Zifuatazo ni hatua ambazo mwalimu atatakiwa kuzifuata kafika kufundisha mada ya "fasihi" kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza.

Hatua ya kwanza kabisa ni Utangulizi Mwalimu atawatambulisha wanafunzi Somo wanaloenda kujifunza kwa siku hiyo kwa kuwaambia mada na Mada ndogo Mfano kueleza kwa kuwaongoza maana ya fasihi au kuwauliza Maswali kuhusiana na kile walichojifunza kipindi kilichopita.

Hatua nyingine ni kuwapa maarifa Mapya. Hapa mwalimu atawaongoza wanafunzi kwa kuwauliza kile wanachoelewa kuhusu fasihi na aina zake na kuchunguza kama wanaweza kueleza kwa usahihi na kufanya marekebisho endapo hawaelewi kwa maelezo kuhusu Mada hiyo. aina za fasihi kwa usahihi.

Kuimarisha maarifa. Hii ni hatua ambayo mwalimu anaifuata kwa kukazia. kile walichojifunza kwa kuwapa



16 maswali kuwauliza kile walicho
jifunza kama wanajibu kwa
usahihi na kurekebisha endapo
wana kosea
Tafakuri: Hii ni hatua amb
ayo mwalimu afundishae fasihi
atafuata kwa kuwapa zoezi
kutokana na mada hiyo Mfano
kuwapa maswali mafano kwa
kila mtu kuyafanya kwenye
daftari yake na mwalimu
kuchunguza ujibuji wao vile
wanavyojibu maswali hayo
kwa usahihi
Hitimisho: Hii ni hatua
ya mwisho ambayo mwalimu
atafuata kwa kuwatumia
wanafunzi wawili kueleza
kwa ufupi walichojifunza.
Siku hiyo au Unaweza Uka
hitimisha mwalimu mwenyewe
wa somo kulingana na somo
ulivyoliona.
Kila mwalimu bora lazima
afuate hatua katika ufundi
shaji mahiri kwani itapelekea
mwalimu huyo kueleweka
na kuwa mwalimu bora
wa somo na atazingatia
matumizi ya muda na zana.

**Kielelezo 16.1** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kubainisha hatua tano zinazotakiwa kufuatwa katika kufundisha mada ya *Fasihi* kwa wanafunzi wa Kidato cha Kwanza kwa ufasaha katika mtiririko mzuri.

Hali kadhalika, asilimia 28 ya watahiniwa walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 5.5. Baadhi yao hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Ufundishaji wa Mada Teule za Somo la Kiswahili*. Vilevile, wengine walishindwa kuelewa mahitaji ya swali na wengine walibainisha hatua za maandalizi ya somo badala ya kujibu hatua za kufuatwa wakati wa kufundisha mada ya fasihi kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza. Kielelezo 16.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyetoa majibu yasiyohusiana na

swali na kusababisha kupata alama hafifu ingawa aliweza kubainisha hatua ya hitimisho na kushindwa kutoa maelezo ya kuridhisha.

**Kielelezo 16.2**


16. Fasihi ni aina ya sanaa inayotumia
lugha kufikisha ujumbe kwa jamii. Zifua-
tazo ni hatua tano za kufuata katika
kufundisha mada ya fasihi kwa
wanafunzi wa kidato cha kwanza,
Kutambulisha maudhui yaliyomo ndani
ya mada hiyo. Hii husaidia wanafunzi
kuelewa mada hiyo inahusu nini.
Kutambua mda utakaotumika katika
kufundishia mada hiyo. Hali hii ita
msaidia mwalimu kufikia lengo
mahususi
Kujua zana itakayotumika, mwalimu
anapaswa kutumia zana inayoendana
na mada.
Pia kuwauliza wanafunzi maswali.
Mwalimu kutoa hitimisho kwa
kuelezea kiundani juu ya mada husika

**Kielelezo 16.2** ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kubainisha hatua zinazotakiwa kufuatwa katika kufundisha mada ya *Fasihi* kwa wanafunzi wa Kidato cha Kwanza kwa ufasaha badala yake alibainisha hatua za maandalizi ya somo.

## 2.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU CHA WATAHINIWA KWA MADA

Mtihani wa 721 Kiswahili ulikuwa na jumla ya maswali kumi na sita (16) yaliyotoka katika mada za *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*, *Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili, Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili, Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili*, *Ufahamu*, *Maendeleo ya Kiswahili, Upimaji, Ufundishaji wa Mada Teule za Somo la Kiswahili, Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili*, *Fasihi, Matamshi* na *Lafudhi ya Kiswahili.*

Uchambuzi wa kufaulu kwa watahiniwa katika mada hizo unaonesha kuwa watahiniwa wamefanya vizuri katika mada 9 ambazo ni sawa na asilimia 82.0 ya mada zilizotahiniwa. Mada hizo ni *Uhakiki wa Kazi za Fasihi (76.6%), Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili (91.3%), Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili (77%), Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili (92.6%), Ufahamu (71.2%), Maendeleo ya Kiswahili (87.6%), Ufundishaji wa Mada Teule za Somo la Kiswahili (72%), Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili (91.8%)* na *Fasihi (83.2%).* Watahiniwa walipata kiwango kizuri cha kufaulu katika mada zilizotajwa, kwa sababu walionesha kuwa na uelewa wa kutosha wa mada zilizotahiniwa na utambuzi sahihi wa matakwa ya kila swali. Hali kadhalika, wengi wao waliweza kujieleza vizuri kwa lugha inayoeleweka, kujenga hoja vizuri katika mtiririko unaoleta mantiki pamoja na kufuata taratibu na kanuni za uandishi hasa katika maswali ya insha.

Aidha, kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika mada ya *Upimaji* kilikuwa cha wastani ambacho ni 63.8% ya mada zilizotahiniwa. Watahiniwa walifaulu kwa kiwango cha wastani katika mada iliyotajwa kutokana na uelewa wa wastani wa mada iliyotahiniwa na kutofuata kanuni za uandishi hususan katika maswali ya insha.

Kwa upande mwingine, uchambuzi ulionyesha kuwa watahiniwa walipata kiwango hafifu katika mada 1 ambayo ni *Matamshi na Lafudhi ya Kiswahili 5.4%* ya mada zilizotahiniwa. Watahiniwa hao walipata kiwango hafifu cha kufaulu katika mada iliyotajwa kutokana na uelewa mdogo wa mada iliyotahiniwa, kutokuelewa matakwa ya swali pamoja na kujibu swali bila

kulikamilisha. Mchanganuo wa viwango vya kufaulu kwa watahiniwa kwa kila mada umefafanuliwa katika viambatisho A na B.

Kwa ujumla, kiwango cha kufaulu cha watahiniwa katika mada ni asilimia 73.8. Hali hii inaonesha kuwa zaidi ya 2/3 ya watahiniwa walikuwa na uelewa mzuri wa mada mbalimbali zilizotahiniwa.

## 3.0 HITIMISHO

Kwa ujumla, mtihani wa 721 Kiswahili mwaka 2018 ulizingatia muhtasari wa somo la Kiswahili. Takribani majazi zote za nyanja ya utambuzi kama vile majazi ya maarifa, ufahamu, matumizi, uchambuzi, uundaji na tathmini zilijidhihirisha dhahiri katika mtihani huo. Aidha, kiwango cha kufaulu kwa ujumla kilikuwa cha kuridhisha ambapo wastani wa kufaulu kwa somo hili ni asilimia 73.8.

Hata hivyo, uchambuzi uliofanyika ulibaini kuwapo kwa changamoto mbalimbali kwa baadhi ya watahiniwa kushindwa kufanya vizuri. Miongoni mwa changamoto hizo ni; uelewa mdogo wa matakwa ya swali, uelewa mdogo wa mada zilizotahiniwa hususan mada ya *Matamshi na Lafudhi ya Kiswahili,* uelewa mdogo wa jinsi ya kujibu maswali na uelewa mdogo wa matumizi ya alama za uakifishaji sambamba na kuandika insha kwa mtiririko wenye kuleta mantiki. Changamoto nyingine iliyobainika ni ile ya baadhi ya watahiniwa kushindwa kutoa mifano sahihi ya kushadidia majibu waliyotoa na kutotii maelekezo ya maswali.

Kwa hiyo, Baraza linatarajia kuwa, changamoto hizo zitatia chachu kwa wakufunzi na walimu tarajali wa somo hili katika kuelewa kasoro zinazofanywa na baadhi ya watahiniwa ambazo husababisha washindwe kujibu vizuri maswali. Kisha, wakufunzi na walimu tarajali waone kuwa kuna haja ya kurekebisha kasoro hizo zilizobainika kwa baadhi ya watahiniwa wa somo hili. Vilevile, taarifa hii itazidi kuchochea ari ya wakufunzi katika kufundisha, kutunga na kusahihisha mazoezi na mitihani mbalimbali ili kuzidi kuinua kiwango cha kufaulu. Kadhalika, walimu tarajali nao wanatarajiwa kuonesha hamasa na ari ya kutaka kuijua na kuimudu lugha ya Kiswahili ambayo inazidi kuenea kwa kasi kote ulimwenguni ili wajijengee umahiri katika kujieleza kwa kujiamni huku wakijivunia kutumia lugha hii.

## 4.0 MAPENDEKEZO

Ili kiwango cha kufaulu katika somo hili kiendelee kuwa juu, inapendekezwa kuwa:

(a) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ione haja ya kuandaa semina kwa wakufunzi wa ndaki za ualimu ili waongeze ujuzi katika mada za *Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili* hususan, katika vipengele vya *elimu matamshi*, *elimu maumbo, elimu miundo na elimu maana*.

(b) Wakufunzi watilie manani katika kuwafundisha na kuwasisitiza walimu tarajali juu ya matumizi sahihi ya alama za uakifishaji sambamba na uandishi wa insha zenye mtitririko wenye kuleta mantiki. Hii itazidi kuchochea kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa ambao wamepata alama hafifu kwa kuandika insha zisizo na mtiririko mzuri.

(c) Wakufunzi na walimu tarajali waone kuwa kuna haja ya kufundisha na kujifunza mada zote kwa kadiri muhtasari unavyoelekeza. Hii inatokana na ukweli kuwa, kuna baadhi ya mada hazikupewa msukumo wa kutosha kwa wakufunzi na walimu tarajali. Mathalani, taarifa hii ilibaini kuwa mada ya *Matamshi na Lafudhi ya Kiswahili* haikupewa msukumo unaostahili.

**KIAMBATISHO A**

## UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU CHA WATAHINIWA KATIKA KILA MADA

| Na | Mada | 2018 | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Namba ya swali | Viwango vya Kufaulu (%) | | Maoni |
| | | | 40 na Zaidi | Wastani | |
| 1 | Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili | 4 | 85.5 | 92.6 | Vizuri |
| | | 15 | 99.6 | | |
| 2 | Vifaa vya Mtalaa wa Somo la Kiswahili | 6 | 91.8 | 91.8 | Vizuri |
| 3 | Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili | 2 | 93.8 | 91.3 | Vizuri |
| | | 14 | 99.6 | | |
| 4 | Maendeleo ya Kiswahili | 8 | 87.6 | 87.6 | Vizuri |
| 5 | Fasihi | 11 | 83.2 | 83.2 | Vizuri |
| 6 | Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili | 3 | 57. 7 | 77 | Vizuri |
| | | 13 | 96.3 | | |
| 7 | Uhakiki wa Kazi za Fasihi | 1 | 88.8 | 76.6 | Vizuri |
| | | 12 | 53.6 | | |
| 8 | Ufundishaji wa Mada Teule za Somo la Kiswahili | 16 | 72 | 72 | Vizuri |
| 9 | Ufahamu | 5 | 71.2 | 71.2 | Vizuri |
| 10 | Upimaji | 9 | 96.1 | 63.8 | Wastani |
| | | 10 | 31.5 | | |
| 11 | Matamshi na Lafudhi ya Kiswahili | 1 | 5.4 | 5.4 | Hafifu |

**KIAMBATISHO B**

**KIWANGO CHA KUFAULU CHA MADA KWA MWAKA 2018**

